**HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA**

**TAARIFA YA UTENDAJI WA SHUGHULI ZA HALMASHAURI KWA MWAKA 2020/2021**

## 1.0 UTANGULIZI.

## 1.1 JIOGRAFIA

Ndugu Wananchi,

Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ni moja kati ya Mamlaka 8 za Serikali za Mitaa zilizo katika Mkoa wa Tabora ambayo inalo eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 14,050 sawa na asilimia 18.8 ya eneo la Mkoa wa Tabora. Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya yapo katika Kata ya Ufukutwa, umbali wa km 125 kutoka Tabora Mjini.

Kiutawala, Wilaya imegawanyika katika tarafa tano (5), Kata 28, Vijiji 99 vilivyosajiliwa na vitongoji 458. Halmashauri ya Wilaya hii inapakana na Wilaya ya Uyui na Wilaya ya Urambo kwa upande wa Mashariki, kwa upande wa Kusini inapakana na Wilaya ya Mlele na Mpanda (Mkoa wa Katavi). Upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Ushetu (Mkoa wa Shinyanga) na Bukombe Mkoa wa Geita na kwa upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Kibondo na Uvinza (Mkoa wa Kigoma).

## 1.2 UCHUMI WA WILAYA

Uchumi wa wilaya hii kwa kiasi kikubwa unategemea sekta kuu mbili (2); Kilimo (70%), Ufugaji (10%). Sekta nyingine ni uvuvi, biashara, na viwanda vidogo vidogo. Kilimo bado kipo katika kiwango cha kujikimu (subsistence) na siyo katika kiwango cha kibiashara. Mazao ya chakula yanayolimwa ni mahindi, mpunga, mhogo, maharage, viazi vitamu, ulezi, mtama na maharage. Mazao ya biashara ni tumbaku, pamba, karanga, alizeti, ufuta, korosho na michikichi.

## 2.0 TAARIFA YA UTENDAJI KAZI WA HALMASHAURI KWA MWAKA 2020/2021

Ndugu Wananchi,

Majukumu yanayotekelezwa na Halmashauri yanalenga katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo iliahidi kutatua changamoto mbalimbali kupitia sekta zilizopo kuanzia ngazi ya chini ambazo zinalenga katika kuboresha maisha ya Wananchi. Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi katika ngazi ya halmashauri unafanyika kupitia Sekta husika kama ilivyobainishwa katika taarifa hii.

## 2.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA 2020/2021

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ilikisia kukusanya na kutumia mapato kutokana na vyanzo vyake vya ndani yenye jumla ya Shs.

3,335,693.660.00. (kati ya makisio hayo Sh.253,299,673.00 yalikuwa ni mapato lindwa na Sh.3,082,394,000.00 yalikuwa ni mapato yasiyo lindwa. Hadi tarehe 30/06/2021, jumla ya Sh. 3,654,320,837.73 zilikuwa zimekusanywa sawa na 110% ya lengo. Kati ya makusanyo hayo

Makusanyo ya mapato yasiyolindwa yaliyoelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo ni Sh. **1,232,957,600.00** sawa na 100%. Aidha kati ya fedha iliyokusanywa Shs 365,432,084 ilielekezwa katika kukopesha vikundi vya Vijana, Wanawake na watu wenye ulemavu sawa na 10%. Matumizi ya fedha iliyoelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SEKTA YA ELIMU

### 2.2.1 IDARA YA ELIMU MSINGI

Wilaya ina jumla ya shule za msingi 108. Hadi Juni, 2021 jumla ya walimu waliopo ni 1,621 ambapo kati yao walimu 1,080 ni wanaume na 541 ni wanawake. Uwiano wa Wanafunzi na walimu ni 80. Aidha Mwezi Mei, 2021 halmashauri imepata usajili wa shule 5 hivyo kuwa na jumla ya Shule 113.

Wilaya ina jumla ya madarasa ya Elimu ya Awali 108 ambayo yote ni ya serikali. Aidha ina jumla ya wanafunzi walioandikishwa hadi sasa wa elimu ya awali ni **16,185** ambapo wavulana ni **8,241** na wasichana ni **7,944.** Jumla ya walimu **118** kutoka Elimu ya Msingi wanatumika kufundisha Elimu ya Awali.

Kwa mwaka 2020/2021 Halmashauri ya Kaliua kupitia Idara ya Elimu imesimamia shughuli zifuatazo: -

i. Usimamizi wa mtihani wa Taifa wa darasa la nne ambapo jumla ya wanafunzi 17,581 walifaulu mtihani wa upimaji Taifa wa darasa la nne sawa na asilimia 88.43 ya wanafunzi waliofanya mtihani. Aidha kwa upande wa mtihani kumaliza elimu ya msingi mwaka 2020, jumla ya wanafunzi 5,637 walifaulu na kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza sawa na asilimia 80.62 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani.
ii. Usimamizi wa taaluma mashuleni umeendelea kufanyika.
iii. Ufuatiliaji wa fedha za elimu bila malipo ambapo Halmashauri kwa kipindi husika ilipokea Sh.876, 388,317.97 zilipokelewa.
iv. Usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za Elimu kupitia program ya elimu ya Kujitegemea ambapo jumla ya vyumba 66 vya madarasa vimeendelea kujengwa kwa kutumia fedha za mapato ya ndani, Wananchi na Wanafunzi. Aidha ujenzi wa vyumba vya madarasa 18 kupitia fedha za ruzuku ya miradi vimejengwa katika shule za msingi za Sasu-1,kapandwashimba-2,making-1,Nsungwa-4,Ibambo-2,Upelle-1,Ikunkwa-2,Changamoto-1,Upendo-2,Igombe-3,Ilege-3,Wachawaseme-1 na Mpwaga-1 ambapo Halmashauri ilipokea Sh.225, 034,334.
v. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na ofisi 3 kupitia program ya EP4R unaendelea katika shule za msingi Kangeme, Mwahalaja na Mnange. Jumla ya Sh.120,000,000.00 zimepokelewa.
vi. Katika kipindi husika jumla ya shule 5 zimeweza kusajiliwa na kufunguliwa. Shule hizo ni Kapandwashimba,Juhudi,Upele,Kakobe na Mgelela

vii. Kuendelea na ujenzi wa miundombinu katika Shule shikizi ili ziwe na vigezo vya kuweza kusajiriwa. Shule hizo ni Ibapa, Muungano na Ibumba

### 2.2.2 IDARA YA ELIMU SEKONDARI

Wilaya ya Kaliua ina jumla ya Shule za Sekondari 20, kati ya hizo 19 za Wananchi na 1 ya binafsi. Kati ya shule hizo shule mbili ni za kidato cha 1-6 ambazo ni Sekondari ya Kaliua na Kashishi. Shule hizi ni za mchepuo wa masomo ya Sayansi.

Hadi Juni, 2021 Halmashauri ilikuwa imesajili wanafunzi **13,212** kati ya hao Wavulana ni **6,800** na Wasichana **6,412** katika shule za Sekondari. Kati ya wanafunzi waliosajiliwa, **489** ni wanafunzi wa kidato cha **5-6** na wanafunzi **12,723** ni wanafunzi wa kidato cha **1-4**.

Halmashauri ina walimu **347**, kati ya hao wanawake ni **85** na wanaume ni **262** Wilaya ya Kaliua ina upungufu wa Walimu **267** katika shule za Sekondari. Upungufu mkubwa wa walimu umejitokeza katika masomo ya Sayansi na Hisabati.

Hali ya Miundombinu ya shule za Sekondari katika Wilaya ya Kaliua haitoshelezi, upungufu mkubwa uko katika nyumba za walimu na vyumba vya madarasa. Kuna jumla ya vyumba 227 vya madarasa kati ya mahitaji ya vyumba 330, Maabara za masomo ya sayansi zipo 57, Nyumba za walimu ni 88 kati ya mahitaji ya nyumba 370, Viti vya wanafunzi vipo 11,869 kati ya mahitaji ya viti 13,212 na meza za wanafunzi zipo 11,556 kati ya mahitaji ya meza 13,212.

Ili kukabiliana na changamoto ya nyumba za Walimu, halmashauri imehamasisha walimu kujenga nyumba za gharama nafuu ambapo kwa sasa takribani asilimia 70 ya walimu wameshajenga nyumba zao

Kwa mwaka, 2020/2021, Halmashauri kupitia idara ya elimu sekondari imetekeleza shughuli zifuatazo;

i. Usimamizi wa mtihani wa kumaliza kidato cha nne ambapo jumla ya Wanafunzi 1,729 walifanya mtihani wa kumaliza elimu ya kidato cha nne kwa mwaka 2020. Kati yao wanafunzi 973 walikuwa ni wa kiume na wanafunzi 756 walikuwa wa kike. Wanafunzi waliofaulu mtihani wa kumaliza kidato cha nne kwa kiwango cha daraja I-IV walikuwa 1,626 sawa na asilimia 94.04 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani.
ii. Usimamizi wa mtihani wa upimaji Kitaifa kidato cha pili ambapo jumla ya Wanafunzi 2,938 walifanya mtihani wa upimaji Kitaifa kidato cha pili kwa mwaka 2020. Kati yao wanafunzi 1,422 walikuwa ni wa kiume na wanafunzi 1,516 walikuwa wa kike. Wanafunzi waliofaulu mtihani wa Taifa wa kidato cha pili kwa kiwango cha daraja I-IV walikuwa 2,811 sawa na asilimia 95.68 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani.
iii. Usimamizi na ufuatiliaji wa fedha za elimu bila malipo ambapo kwa kipindi husika halmashauri imepokea jumla ya Sh.442,256,932.16
iv. Usimamizi wa ujenzi wa miundombinu ya kutolea elimu ya sekondari ambapo kupitia program ya elimu ya Kujitegemea halmashauri imeendelea kujenga vyumba 47 vya madarasa kupitia vyanzo vya mapato ya ndani, wananchi na wanafunzi.
v. Halmashauri imeendelea na ujenzi/ukamilishaji wa vyumba 12 vya maabara za masomo ya sayansi ambapo jumla ya Sh.360,000,000.00 zilipokelewa na utekelezaji uko katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:
   -Vyumba 2 vya maabara Sekondari ya Seleli vimekamilika
   -Vyumba 2 vya maabara Sekondari ya Zugimulole vimekamilika

-Vyumba 2 vya maabara sekondari ya Silambo vimekamilika na 1 kiko hatua za mwisho za ukamilishaji

-Chumba 1 cha maabara sekondari ya Ilege kimepakwa rangi

-Vyumba 2 vya maabara sekondari ya Dkt John Pombe magufuri vimepigwa ripu na kufungwa Gypsum board

-Vyumba 2 vya maabara sekondari ya Igwisi vimepakwa rangi

-Vyumba 2 vya maabara Kanoge vimepigwa ripu na kujengwa meza

vi. Ujenzi wa bwalo la chakula katika sekondari ya kashishi unaendelea na uko hatua ya upigaji wa ripu na ukarabati wa daharia katika sekondari ya Mkindo uko hatua ya upigaji wa ripu. Aidha, ujenzi wa jengo la utawala katika shule ya sekondari DKT John Pombe Magufuri uko katika hatua ya uwekaji wa Aluminium, blundering na skiming. Miradi hii inatekelezwa kupitia vyanzo vya mapato ya ndani.

vii. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa na ofisi katika shule za sekondari kashishi-2, Igagala-2 na Usinge-2 uko hatua ya ukamilishaji kupitia program ya P4R ambapo Halmashauri ilipokea kiasi cha Sh.120,000,000.00

viii. Usimamizi wa mara kwa mara wa taaluma mashuleni umeendelea kufanyika.

ix. Halmashauri imefanikiwa kusajili na kufungua Shule 1 ya Sekondari ya kata ya Kamsekwa yenye Jina la Dkt John Pombe Joseph Magufuli.

x. Kuanza ujenzi wa sekondari mpya katika katika maeneo ya Usenye, Kasungu, Mpandamlowoka, Konanne na making. Sekondari ya Usenye ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa boma limekamilika, Kasungu ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na ofisi boma limekamilika, Mpandamlowoka-Ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa boma limekamilika na matundu 10 ya vyoo ujenzi unaendelea, Konanne-ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa viko hatua ya boma na Makingi-ufyatuaji wa tofari umefayika na maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa msingi yanaendelea.

xi. Utekelezaji wa program ya Elimu ya kujitegemea unaendelea ambapo shule zinaendelea na ufyatuaji wa tofari.Niwahimize Wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha ili changamoto ya miundombinu katika shule za Msingi na sekondari iweze kupunguzwa.

## 2.3 SEKTA YA AFYA:

Wilaya ya Kaliua ina jumla ya vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 48. Kati ya hivyo, vituo 41 ni vya Serikali, vituo 2 vinamilikiwa na taasisi za kidini na vituo 5 ni vya watu binafsi.

Kati ya vituo vya Serikali vya kutolea huduma za Afya vilivyopo kuna Hospitali 1 ya Wilaya, Vituo vya Afya 3 na Zahanati 37. Kwa upande wa vituo vinavyomilikiwa na taasisi za kidini na watu binafsi kuna Hospitali 1 na Zahanati 6.

Hata hivyo kuna zahanati 3 ambazo zimekamilika na taratibu za kuziombea usajili zinaendelea. Zahanati hizo ni Ichemba, Usangi na King’wangoko. Aidha Zahanati 3 pia ziko katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa miundombinu. Zahanati hizo ni Usonga, Igombe, Utantamke na Luganjomtoni.

Idara ina jumla ya watumishi 186 wanaotoa huduma katika vituo hivyo vya kutolea huduma. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 30 ya mahitaji halisi ya Wilaya (627). Upungufu huu mkubwa unaathiri hali ya utoaji wa huduma za afya katika vituo vyetu

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021, Halmashauri ya Wilaya ya kaliua kupitia sekta ya afya imetekeleza shughuli zifuatazo; -

i. Usimamizi wa usambazaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za Afya vya Serikali umefanyika. Kwa sasa hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo ni asilimia 94. Manunuzi ya dawa yamekuwa yakifanyika kupitia vyanzo vya fedha vya Mfuko wa pamoja wa Afya (HBF), NHIF, CHF, malipo ya papo kwa papo na ruzuku kutoka Wizara ya Afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Kwa sasa MSD inaendelea kusambaza dawa (mzunguko wa tano na wa sita) katika vituo vya kutolea huduma ambapo hadi kufikia tarehe 6 Juni, 2021 jumla ya vituo 29 vimepelekewa dawa kutoka MSD.

ii. Utoaji wa huduma za Matunzo kwa wagonjwa wanaoishi na Maambukizi ya VVU kupitia vituo 42 vya kutolea matunzo (CTC) kwa wateja wanaoishi na VVU na UKIMWI na vituo vitatu kupitia huduma za mkoba. Jumla ya wateja **17,632 wamewahi kuandikishwa** wanapata huduma za CTC ambapo **10,534** ni wanaume na **7,098** ni wanawake. Wateja walio kwenye dawa za kupunguza makali ya V.V.U ni **21,269** ambapo **13,178** ni wanaume na **8,091** ni wanawake. Idadi hii ya wanaotumia dawa za kufubaza nguvu za VVU ni pamoja na wale ambao waliwahi kusajiriwa katika Wilaya hii. Mfano ni wateja wanaoishiwa dawa wakiwa safarini. Watoto wanaopata huduma ya CTC ni 898 ambapo 518 ni wavulana na 471 ni wsichana. Watoto walio kwenye dawa za kupunguza makali ya VVU ni 1,280.

iii. Usimamizi wa ukamilishaji wa zahanati 4 katika Vjiji vya Shella, Usonga, Igombe, na utantamke unaendelea na zahanati hizi ziko katika hatua za mwisho za ukamilishaji ambapo halmashauri imepokea jumla ya Sh.200,000,000.00 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati hizo.

iv. Ujenzi wa kituo cha afya usinge unaendelea ambapo jumla ya Sh.500, 000,000.00 zimepokelekwa kutoka Serikali Kuu. Majengo yanayoendelea kujengwa na hali halisi ya utekelezaji ni akam ifuatavyo;-
   - Ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD)- hatua ya skiming na upakaji rangi
   - Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa ndani (IPD)-hatua ya blundering na upigaji ripu
   - Ujenzi wa jengo la upasuaji-hatua ya blundering na upigaji ripu
   -Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti-limepigwa ripu na kufanyiwa skiming.

v. Ujenzi wa kituo cha Afya Uyowa ambapo jumla ya sh.600,000,000.00 zimepokelewa. Utekelezaji wa mradi huu ni kama ifuatavyo;
   -Ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wan je (OPD)-limefanyiwa skiming
   -Ujenzi wa jengo la wagonjwa wa ndani (IPD)-limepauliwa
   -Ujenzi wa jengo la upasuaji-limepauliwa na kuwekwa dari
   - Ujenzi wa jengo la kuhifadhia maiti -limepaulilwa na kuwekwa dari.

vi. Ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambapo jumla ya Sh.1,000,000,000.00. majengo yanayoendelea kujengwa ni pamoja na ukamilishaji wa jengo la wagonjwa wa nje, Maabara, Wodi ya watoto na kichomea taka na ujenzi wa Wodi ya Wanaume, Wodi ya watoto na jengo la kuhifadhia maiti. Majengo haya yako katika hatua za mwisho za kukamilishwa.

## 2.4 SEKTA YA KILIMO

Wilaya ya Kaliua ina jumla ya eneo la kilomita za mraba 14,050 sawa na hekta 1,405,000 na kati ya hizo takriban hekta 196,550 zinafaa kwa shughuli za kilimo sawa na asilimia 12 ya eneo lote la Wilaya. Eneo linalolimwa ni Ha 150,000 sawa na asilimi 76.3 ya eneo linalofaa kulimwa. Kilimo ni shughuli iliyoajiri zaidi ya 80% ya wakazi wa wilaya ya Kaliua. Shughuli hii pia ni mhimili mkubwa wa usalama wa chakula na

kipato. Hivyo uchumi waWilaya hii kwa sehemu kubwa unategemea sana kilimo. Wastani wa kiwango cha mvua kwa mwaka ni mm 795.1 hadi mm 1,262.8.

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021, Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika imesimamia na kutekeleza shughuli mbalimbali za Kilimo katika Kata 28 za wilaya ya Kaliua kama ifuatavyo; -.

i. Kuratibu na Kushiriki maadhimisho ya sherehe za nanenane kanda ya magharibi ambapo Halmashauri ilishika nafasi ya pili kwa ushindi wa jumla Kikanda.
ii. Kusimamia masoko ya tumbaku na pamba kwa msimu wa 2020 ambapo kiasi cha pamba iliyonunuliwa ni kilo 580,880 na tumbaku kilo 5,720,568.97.
iii. Kupitia maafisa ugani waliopo ngazi ya kata, wakulima wapatao 1,680 wa mazao ya bustani wamesimamiwa na kupewa ushauri.
iv. Uhamasishaji wakulima kufanya maandalizi ya kilimo kwa mazao ya chakula na biashara kwa msimu wa kilimo 2020/2021.Uhamasishaji umefanyika kupitia mikutano iliyoongozwa na Viongozi kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, halmashauri, Chama Kikuu cha Milambo na viongozi wa vyama vya msingi katika kanda tatu za uzalishaji (Kaliua - Kasungu Amcos, Igagala –Chimbuko Amcos, Ulyankulu-Amahoro AMCOS).
v. Kutoa elimu ya ukadiriaji wa mahitaji ya chakula kwa kaya na uhifadhi, wakulima kupitia mikutano wamepewa, elimu ya ukadiliaji na uhifadhi wa chakula ili kuepukana na upungufu wa chakula ngazi ya kaya.
vi. Idara ya kilimo kupitia ofisi ya ushirika, kwa kipindi hiki imesimamia malipo yote ya mazao ya Tumbaku na Pamba kuhakikisha wakulima katika vyama vyote wanapata staiki zao hadi kufikia Juni, 2021, Makampuni yote yalikuwa yamekamilisha kulipa wakulima yalikuwa mawili ambayo ni JTI na Alliance one. Kampuni ya MAGEFA na GRAND TOBACO TANZANIA LTD bado hayajakamilisha malipo kwa wakulima na ushuru wa Halmashauri.
vii. Umefanyika ukaguzi wa mahesabu katika vyama vya Uhindi, Ugunga na Isenga**.**
viii. Kufanya mikutano ya usuluhishi kwa vyama vya msingi vyenye migogoro ambavyo ni Chimbuko Amcos, Usaguzi Amsos, Uhindi Amcos, Ugunga na Tuinuane Amcos.
ix. Kwa kushirikiana na taasisi ya utafiti TARI Tumbi tumefanikiwa kufanya ziara kwa muda wa siku tano kwa lengo la kuwatembelea wakulima ili kuwapa elimu ya uzalishaji wa zao la michikichi. Jumla ya wakulima 12 katika kata za ufukutwa, Limbula, Kazaroho, Ushokola walitembelewa na kupewa mafunzo kwa vitendo.
x. Jumla ya maafisa uganii 7 na wakulima 4 walipata mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho, mafunzo haya yaliendeshwa na kituo cha utafiti wa kilimo Naliendele
xi. Idara kwa kushirikiana na maafisa ugani na watendaji wa vijiji imeandaa malengo ya uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula kwa msimu 2020/2021
xii. Kusimamia malipo ya Wakulima wa Pamba ambapo Sh.70,956,444.00 zilipokelewa na kulipwa kwa wakulima waliokuwa wanastahili.
xiii. Usimamizi wa masoko ya Tumbaku kwa msimu wa 2021 ambapo masoko yalizinduliwa tarehe 29/04/2021 na kwa sasa jumla ya Makampuni 5 yenye vibali na leseni yapo sokoni kwa ajili ya ununuzi wa Tumbaku ambapo hadi masoko yanafungwa jumla ya kilo 8,963,818zilikuwa zimenunuliwa kutoka kwa wakulima kwa wastani wa bei kati ya Dolla 1.4 hadi Dolla 2.
xiv. Usimamizi wa masoko ya pamba ambayo yamezinduliwa tarehe 21/05/2021 yanaendelea kufanyika ambapo kuna jumla ya Kampuni 4 ambazo zina vibali. Hadi sasa Jumla ya kilo 799,370 zimenunuliwa kutoka kwa wakulima.

xv. Kuondoa tozo ya kuni ya Sh.50, 000 kwa kila mkulima wa Tumbaku ambapo wakulima wa Tumbaku walikuwa wanakatwa na fedha kuelekezwa katika Vijiji na Kata kwa ajili ya Shughuli za maendeleo. Kwa sasa Uchangiaji wa wananchi katika shughuli za maendeleo utafanyika kwa kuzingatia maazimio yaliyokwisha pitishwa na Baraza la madiwani na kadili ya Wananchi watakavyokubaliana katika Vikao vyao.

## 2.5 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Kwa mwaka, 2020/2021, halmashauri ya Wilaya ya kaliua kupitia Idara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza shughuli mbalimbali zilizolenga kutoa huduma za ugani zenye ubora na kuwasaidia wafugaji kuinua kipato chao kama ifuatavyo; -

i. Usimamizi wa uchinjaji wa nyama ambapo jumla ya ng'ombe 2,644, mbuzi 1,468, kondoo 75 na nguruwe 186 walichinjwa na kukaguliwa.
ii. Elimu na hamasa ya uogeshaji wa mifugo ili kuwakinga na magonjwa yaenezwayo na kupe imetolewa kwa wakulima ambapo jumla ya ng'ombe 4,045; mbuzi 393; kondoo 60; mbwa 195 waliogeshwa.
iii. Utoaji wa elimu ya ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ya kuchimba umefanyika kwa wafugaji 3 katika kata za Ugunga, Kazaroho na Ushokola wamefikiwa na kupewa elimu ya uchimbaji na ufugaji wa samaki kwenye mabwawa ya kuchimba.
iv. Usimamizi wa biashara ya mifugo ulifanyika katika minada 8 ya Ugansa, Upele, Mkuyuni, Wachawaseme, Zugimlole, Mwamnange, Ulyankulu na King'wangoko.
v. Ukusanyaji wa Mapato yatokanayo na tozo za ushuru na vibali ulifanyika kama ifuatavyo:
   a) Maduhuli ya Serikali kuu (Vibali vya Usafirishaji wa Mifugo): Jumla ya Tshs. 57,462,500/= zilikusanywa.
   b) Ushuru wa Halmashauri (Minada): Jumla ya Tshs. 82,182,000/= zilikusanywa.
   c) Ushuru wa Leseni za Uvuvi/Vibali vya samaki/Vibali vya Porini: Jumla ya Tsh. 17,334,200/= zilikusanywa.
vi. Ukaguzi na usajili wa maduka ya kuuzia pembejeo za mifugo 42 umefanyika na wamiliki kuelekezwa kufanya shughuli zao katika mazingira yanayo zingatia sheria, taratibu na kanuni zilizowekwa.
vii. Kuratibu na kusimamia mradi wa ukarabati wa josho la Kazaroho ambapo ukarabati wa sakafu, ukuta, tanki la kuchanganyia dawa, birika la kunyweshea maji mifugo, uwekaji mageti ya chuma na upauaji umefanyika na kukamilika.
viii. Kufanya utafiti wa uwepo wa mbung'o wenye vimelea vya ndorobo na malale kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Kituo cha utafiti wa Wadudu Wasumbufu kilichopo Arusha (Tropical Pesticide Research Institute) katika vijiji 2 vya Lumbe na Usinga. Utafiti huu umefanyika katika hatua ya awali ambapo hatua inayofuata ni kuchukua sampuli za damu kwa ajili ya uchunguzi. Uwekaji wa mikakati ya udhibiti wa Mbung'o utategemea kiwango cha maambukuzi ya Vimelea vya Ndorobo kwa Binadamu na Wanyama.

## 2.6 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Kwa mwaka, 2020/2021, Halmashauri ya Kaliua kupitia Idara ya maendeleo ya Jamii imetekeleza shughuli zifuatazo;

i. Uhakiki wa vikundi vilivyokopeshwa mikopo katika Kata zote. Jumla ya vikundi 119 vilihakikiwa ikiwa ni vikundi vya Wanawake-65, Vijana-42 na Walemavu-12.

Jumla ya vikundi 115 vilipata sifa ya kupatiwa mikopo. Hata hivyo kutokana na upungufu wa fedha ni vikundi 45 tu ndio viliweza kukopeshwa.

ii. Uwezeshaji wa vikundi vya uzalishaji mali 68 umefanyika ambapo jumla ya Sh.560,000,000.00 zimetolewa kwa vikundi 28 vya Wanawake (Sh. 231,800,000.00), Vikundi 27 vya Vijana (Sh. 291,200,000.00) na Vikundi 13 vya Walemavu (Sh.37,000,000).
iii. Ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwa vikundi vilivyokopeshwa umefanyika ambapo kwa kipindi cha hadi Juni, 2021 jumla ya Sh. 425,413,000.00 zimerejeshwa ambapo kati yake Sh. 270,846,700.00 ni kutoka katika Vikundi vya Wanawake, Sh. 150,616,300.00 kutoka vikundi vya Vijana na Sh. 3,950,000.00 ni kutoka katika vikundi vya walemavu.
iv. Kufanya uhakiki kwa Kaya 7,168 ambapo Kaya 5,586 katika Vijiji 54 zilihakikiwa na kuwezesha kupitia program ya TASAF. Jumla ya Sh 1,130,682,000.00 zimehawilishwa kwa Kaya husika.
v. Utambuzi wa awali wa Kaya masikini katika Vijiji 78 umefanyika ambapo jumla ya Kaya 18,123 zilitambuliwa.
vi. Kuendelea na uhakiki wa kaya 2,127 za walengwa ambazo zilikuwa zimebaki katika zoezi la awali.

## 2.7 SEKTA YA ARDHI NA MALIASILI

Kwa mwaka, 2020/2021 Halmashauri kupitia Idara ya Ardhi na Maliasili imetekeleza shughuli zifuatazo;

i. Uandaaji wa michoro ya mipangomiji mitatu ambayo iliwasilishwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Mipangomiji Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya makazi.
ii. Upimaji wa viwanja 99 kupitia zoezi la urasimishaji makazi holela katika eneo la Kaliua Mashariki, Kaliua magharibi na Kawawa na Wananchi wanaendelea kumilikishwa.
iii. Uandaaji wa hati 4 za viwanja na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Jumla ya Sh.8,058,736 zimekusanywa kutokana na mauzo ya Viwanja. Aidha deed plan ya kijiji cha Tuombemungu imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Kamishina kwa ajili ya kuidhinishwa.
iv. Uthamini wa eneo la kutupa taka ngumu, taka maji na eneo la makaburi umefanyika. Kinachosubiriwa ni taarifa ya mwisho ya Mthamini ili taratibu nyingine ziweze kufanyika.
v. Ukataji na uchimbaji wa visiki katika maeneo yanayotarajia kuchongwa barabara katika Viwanja vya eneo la Kasungu ambapo jumla ya km 11.44 zimeondolewa visiki na barabara yenye urefu wa km 3.2 imechongwa na taratibu za kupata greda kwa ajili ya uchongaji wa eneo lililobaki zinaendelea. Katika shughuli hii jumla ya Sh 18,484,910.00 zimetumika kulipa vibarua na wasimamizi wa kazi.
vi. Upimaji wa awali wa viwanja kwa ajili ya kurasimisha makazi holela katika eneo la Ugansa.Mchoro wa mipangomji (TP) umeandaliwa na kazi inayoendelea kwa sasa ni utambuzi wa maeneo ambapo baada ya zoezi hilo kukamilika litafuatiwa na zoezi la upimaji wa viwanja ambapo kila kiwanja kinatakiwa kulipiwa Sh.70,000.00 kwa awamu tatu. Kwa hatua za awali jumla ya fedha iliyotumika kutoka halmashauri ni Sh.12, 350,000.
vii. Kuanza mchakato wa kubadili matumizi ya Hifadhi ya Msitu wa Ulyankulu kutokana na maeneo mengi yam situ kuwa yameharibiwa. Tathimini ya awali imeshanywa na Wataalam kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI wakishirikiana na wataalam wa Halmashauri.

## 2.8 SEKTA YA USAFI NA UDHIBITI TAKA NGUMU

Kwa mwaka 2020/2021, Halmashauri imesimamia mambo kupitia Idara ya Usafi na udhibiti wa taka ngumu, yafuatayo; -

i. Kusimamia mchakato wa upatikanaji wa Mzabuni wa kufanya usafi katika Mji wa Kaliua na eneo la Ulyankulu. Shughuli za usafi katika mji wa Kaliua, Ushokola na Ulyankulu zimebinafsishwa kwa sasa zinafanyawa na Kikundi cha FPF.
ii. Kusimamia shughuli za usafi wa mazingira kwa kila Jumamosi na Jumamosi ya Mwisho wa mwezi. Pia jamii imeendelea, kuhamasishwa juu ya umuhimu wa usafi wa mazingira na utoaji wa elimu juu ya umuhimu wa usafi na uhifadhi wa mazingira. Elimu imetolewa katika kata 8 ambazo ni Kaliua, Ufukutwa, Ushokola, Usinge, Usenye, Uyowa, Silambo na Mwongozo
iii. Kusimamia ufanyikaji wa Tathimini ya athari ya kimazingira (Environment audit) imefanyika kwenye kituo cha kuuzia mafuta cha Kaliua check point.
iv. Usimamizi wa Kitalu cha Halmashauri cha miti ya matunda, kivuli na mbao kimeanzishwa, na jumla ya miti 100,125 imeoteshwa
v. Vituo 2 vya kuuzia mafuta, mashine 8 za kusaga nafaka na kukoboa, na mashine 6 za kulanda mbao zimekaguliwa na wamiliki walipewa maelekezo juu ya kuimarisha hali usafi, afya na usalama mahali pakazi.

## 2.9 SEKTA YA UTAWALA NA FEDHA

Kwa mwaka, 2020/2021, Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua kupitia idara za Utawala na Fedha imeweza kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Halmashauri imepokea watumishi wapya 76, kati yao Idara ya Afya 2, Elimu sekondari 12, Elimu msingi 59 na Ujenzi 2.
ii. Katika kipindi husika jumla ya watumishi 7 wamestaafu, 4 wamefariki, 31 wamehama kwenda Halmashauri na taasisi nyingine za Serikali na watumishi 9 wamehamia Wilaya ya Kaliua
iii. Kushughulikia madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi ambapo jumla ya Watumishi (96) wamelipwa kiasi cha Tsh 88,712,300
iv. Kuandaa na kuingiza madeni mbalimbali ya walimu zikiwemo nauli za likizo ,uhamisho, matibabu na nauli kwa Ajira mpya kwenye mfumo wa madeni uitwao Madeni MIS.
v. Matengenezo ya magari yameendelea kufanyika kwa kuzingatia bajeti.
vi. Menejimenti imefanya ununuzi wa gari Double Cabin baada ya kulipwa fidia na kampuni ya bima Sh.87, 400,000.00 kutokana na gari aina ya Double Cabin lililopata ajali. Gari limekwisha wasili na linatoa huduma.
vii. Upandishaji wa madaraja kwa watumishi 1,540 wa kada mbalimbali.
viii. Usimamizi wa vikao mbalimbali kuanzia ngazi za Vitongoji, Vijiji, Kata na Wilaya kwa lengo la kuimarisha Utawala bora.
ix. Kuratibu taarifa za Watumishi waliopo masomoni kwa mwaka wa Fedha wa 2019/2020 na 2020/2021, waliomaliza masomo katika kwa kipindi cha mwaka 2017/2018 hadi mwaka 2019/2020 na taarifa ya watumishi wote waliotoka masomoni.

x. Kusimamia mchakato wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti ya halmashauri kwa mwaka 2021/2022 ambapo Bajeti imeidhinishwa na Bunge na imeanza kutekelezwa. Hivyo niwaombe Wananchi wajipange katika maeneo yao kwa kuchangia miradi ili fedha zitakapokuja ziweze kutekeleza miradi kwa tija zaidi.
xi. Uandaaji wa Hesabu za Mwisho za Halmashauri (Final Account) na kitabu cha LAAC pamoja na kutekeleza mapendekezo ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Mkaguzi wa ndani. Vitabu vya taarifa husika vimekamilika na kuwasilishwa ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
xii. Kuendelea na uratibu wa wawekezaji wa Sekta Binafsi wanaowekeza katika Wilaya yetu na wanachangia katika ukuaji wa Mji wa kaliua na Viunga vyake.
xiii. Mchakato wa uanzishwaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ulyankulu unaendelea ambapo kwa sasa utoaji wa maoni kwa ngazi ya chini unaendelea na kasha baada ya hapo hatua nyingine zitaendelea.

## 3.0 UCHANGIAJI WA WANANCHI KATIKA SHUGHULI ZA MAENDELEO

Ndugu Wananchi,
Maendeleo ya kweli ni yale ambayo Wananchi wanashiriki kuyaleta kupitia ushiriki wao wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika maeneo yao. Niyapongeze maeneo ambayo wanajitoa kikamilifu na matokeo chanya yanaonekana. Hata hivyo kuna maeneo ambayo ushiriki wa Wananchi katika shughuli za maendeleo ni hafifu hivyo kuyapelekea maeneo hayo kuwa nyuma kimaendeleo.

Ni dhahiri kuwa fedha zinazoletwa kutoka Serikali kuu kwa ajili ya shughuli za maendeleo haiwezi kutosheleza hivyo Kupitia kikao hiki,niwahimize Wananchi wote tushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo katika maeneo yetu ili kuweza kuleta mabadiliko chanya na tupuuze baadhi ya Wanasiasa wanaochochea Wananchi kutochangia shughuli za maendeleo kwani watatuchelewesha kuleta maendeleo katika maeneo yetu.

## 4.0 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI HALMASHAURI KATIKA UTENDAJI WA SHUGHULI

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2020/2021, kuna changamoto mbalimbali zinazotukabili ikiwa ni pamoja na; -

i. Uhaba wa miundombinu ya kutolea huduma za elimu kwa upande wa shule za msingi na sekondari hususani vyumba vya madarasa.
ii. Uhaba mkubwa wa watumishi hususani wa Kada ya Afya, walimu hususani wa masomo ya Sayansi, kilimo na Mifugo.
iii. Kutopatikana kwa baadhi ya dawa na vifaa tiba kutoka MSD hivyo kusababisha vituo vingi kutokuwa na dawa husika kwa muda mrefu hivyo kupelekea usumbufu mkubwa kwa wateja kutokana na taratibu za manunuzi.

iv. Mwitikio mdogo wa wananchi katika kushiriki kwenye mikutano ya kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya mbinu mbalimbali za kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI.

## 4.1 MIKAKATI YA KUINUA KIWANGO CHA ELIMU YA MSINGI

Ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza, Halmashauri imefanya yafuatayo; -

i. Kuendelea kutenga bajeti ya watumishi hususani katika sekta ya elimu, Afya, Kilimo na Maendeleo ya Jamii.
ii. Kuendelea kuhamasisha Wadau mbalimbali ikiwemo Wananchi ili kujenga miundombinu ya kutolea huduma za elimu.
iii. Kuendelea kuhamasisha Wananchi ili waweze kupima na kutambua afya zao.

**HITIMISHO**

Ndugu Wananchi,

Nichukue fursa hii kuwashukuru Wadau wote wanaoshiriki kwa njia moja ama nyingine katika kuleta Ustawi wa Watu wa Kaliua, Nimshukuru Mkuu wa Wilaya yetu Ndugu Paulo Matiko Chacha na kamati yake ya Usalama ya Wilaya, Chama Cha Mapinduzi na vyama rafiki, Wah. Madiwani wote, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Timu yake na Wananchi wote kwa ujumla, kwani pamoja na Changamoto zinazojitokeza tumeendelea kuwa wamoja katika kuzitatua.

Mwisho, niwaombe tuendelee kuwa wamoja, tufanye kazi kwa juhudi kubwa katika maeneo yetu ili tuweze kuleta mabadiliko Chanya katika Halmashauri yetu.

***Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Tabora, Mungu Ibariki Kaliua***